Kiswahili | سواحلي | فَضْلُ عَشْرِ ذِي الحِجَّةِ

# FADHILA ZA SIKU KUMI (ZA MWANZO) ZA DHUL-HIJA

Kamati ya Kielimu ya usimamizi wa mambo ya Dini
ya Msikiti Mtukufu wa Makkah na Madinah

ⓒجمعية خدمة المحتوى الإسلامي باللغات ، ١٤٤٨هـ

جمعية خدمة المحتوى الإسلامي باللغات
فضل عشر ذي الحجة - سواحيلي. / جمعية خدمة المحتوى
الإسلامي باللغات - ط١. .- الرياض ، ١٤٤٨هـ
١٤ ص ؛ ..سم

رقم الإيداع: ١٤٤٨/٥٦١٤
ردمك: ٣-٥١٧-٥١٧-٦٠٣-٩٧٨

# فَضْلُ عَشْرِ ذِى الحِجَّةِ

# FADHILA ZA SIKU KUMI (ZA MWANZO) ZA DHUL-HIJA


اللَّجْنَةُ العِلْمِيَّةُ

بِرِئَاسَةِ الشُّؤُونِ الدِّينِيَّةِ بِالمَسْجِدِ الحَرَامِ وَالمَسْجِدِ النَّبَوِيِّ

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

# FADHILA ZA SIKU KUMI (ZA MWANZO) ZA DHUL-HIJA

## Utangulizi

Kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu, na rehema na amani zimfikie yule aliyetumwa kuwa rehema kwa walimwengu, na kwa watu wake, na Maswahaba zake, na wale waliofuata mwenendo wake, na wakaongoka kwa muongozo wake, mpaka siku ya Malipo. Ama baada ya hayo:

Huu ni ujumbe mfupi, uliokusanya mambo muhimu anayoyahitaji Muislamu katika fadhila za siku kumi za mwanzo wa Dhul-Hija. Tumezikusanya kwa ajili ya mwenye kutembelea Misikiti Miwili Mitukufu, mwanaume na mwanamke; ili wawe na elimu na utambuzi na mambo ya dini yao, tukitaraji kutoka kwa Mkarimu, Mwingi wa kuneemesha awanufaishe kwa ujumbe huu, na aufanye kuwa wenye kufaa, na uwe kwa ajili ya kutaka uso wake tu. Kwani, Yeye ndiye mbora wa wenye kuombwa na Mkarimu zaidi anayetarajiwa.

Kamati ya Kielimu ya Jumuia ya Kuhudumia Maudhui za Kiislamu kwa Lugha Mbalimbali.

## Fadhila za siku kumi (za mwanzo) za Dhul-Hija:

Siku kumi (za mwanzo) za Dhul-Hija, ubora wake ni mkubwa mno. Ameubainisha Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kitabu chake, na akaubainisha Mtume wake Muhammadi, rehema na amani ziwe juu yake, katika mafundisho yake. Nazo ndizo zile siku ambazo ameapa kwazo Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya Kitabu chake katika kauli yake:

﴿وَٱلۡفَجۡرِ ١ وَلَيَالٍ عَشۡرٖ ٢﴾

***"Ninaapa kwa (wakati wa) Alfajiri ****

***Na kwa usiku kumi wa mwanzo (wa Mfungotatu, Dhul-Hija)."*** [Surat Al-Fajri: 1-2] Nazo ni siku kumi (za mwanzo) za Dhul-Hija, kama alivyosema (Abudllahi) bin Abbas, (Abdullahi) bin Zubairi, Mujahid, (umamu) bin Kathiri, (imamu) bin Al-Qayyim na zaidi ya mmoja katika wema waliotangulia na wale waliofuata baada yao.[1]

Nazo ni siku ambazo kufanya matendo ndani yake huwa bora zaidi kuliko hata kupigana vita katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; kwa hadithi ya (Abdullahi) bin Abbas, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao, kwamba alisema: Alisema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake: "Hakuna siku ambazo kufanya matendo mema ndani yake hupendeza zaidi kwa

---

[1] Tazama Tafsiri bin Kathiri 4/106, na Zaadul-Ma'aadi 1/56.

Mwenyezi Mungu kuliko hizi siku kumi." Wakasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hata kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu?" Akasema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake: "Hata kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa mtu aliyetoka kwa nafsi yake na mali yake, na akawa hakurudi na chochote katika hivyo."[1]

## Matendo bora zaidi katika siku kumi (za mwanzo) za Dhul-Hija:

1- Kutekeleza Hija na Umra. Haya ni katika matendo bora zaidi ndani ya siku kumi hizi; kwa kauli ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake: "Atakayehiji na akawa hakusema maneno machafu wala kutenda matendo machafu, anarudi kama siku aliyozaliwa na mama yake (akiwa hana dhambi)." Na katika tamko la Muslim: "Atakayeiendea nyumba hii, na akawa hakusema maneno machafu wala kutenda matendo machafu, anarudi kama siku aliyozaliwa na mama yake (akiwa hana dhambi)."[2] Kauli yake: "Atakayeiendea nyumba hii" inajumuisha kwa muktadha wake Hija na Umra, na kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu. Na amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake. "Kufanya Umra mpaka Umra nyingine kunafanya mtu kusamehewa madhambi

[1] Kaipokea Bukhari, na Tirmidhi na tamko hili ni lake.
[2] Kaipokea Bukhari na Muslim.

yanayofanyika baina ya Umra hizo mbili. Na Hija iliyokubalika haina malipo isipokuwa Pepo."[1]

2- Kufunga siku tisa (za mwanzo za Dhul-Hija) au zitakazowezekana katika hizo. Hili ni kwa kauli ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake: "Hakuna siku ambazo kufanya matendo mema ndani yake hupendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko hizi siku kumi." Na swaumu ni miongoni mwa matendo mema matukufu zaidi ambayo alihimiza Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, na akahamasisha juu yake. Miongoni mwake ni kauli yake, rehema na amani ziwe juu yake: "Hakuna mja yeyote atakayefunga siku moja katika njia ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa Mwenyezi Mungu atauweka mbali kwa siku hiyo moja uso wake na moto misimu sabini."[2]

3- Ni sheria kuchinja udhuhiya siku ya kuchinja na siku za Tashriiq (kubanika nyama). Imethibiti kuwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake: "Alichinja siku ya Idi kondoo wawili weupe wenye pembe. Aliwachinja kwa mkono wake, ataja jina la Mwenyezi Mungu juu yake, akatoa takbira na akaweka mguu wake juu ya shingo zao."[3]

Na imesimuliwa kutoka kwa Aisha, radhi za

---

[1] Kaipokea Bukhari na Muslim.
[2] Ameipokea Bukhari na Muslim.
[3] Ameipokea Bukhari na Muslim.

Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kwamba alisema: Alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani ziwe juu yake: "Hajawahi kufanya mwanadamu tendo lolote siku ya kuchinja (siku ya Idi) linalopendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko kumwaga damu. Na hakika kitaletwa kichinjwa hicho siku ya Kiyama kikiwa na pembe zake, nywele zake na kwato zake. Na hakika damu hiyo hufika kwa Mwenyezi Mungu katika mahali (pa kukubalika) pake kabla haijadondoka katika Ardhi. Basi zisafisheni kwavyo (vichinjwa) nafsi zenu."[1]

Na zinapoingia siku kumi (za mwanzo) za Dhul-Hija; atajizuia aliyekusudia kuchinja kunyoa nywele zake na ngozi yake; kwa mujibu wa hadithi ya Ummu Salama, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kutoka kwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, ya kwamba alisema: "Mtakapouona mwezi mwandamo wa Dhul-Hija, na akataka mmoja wenu kuchinja; basi ajizuie kunyoa nywele zake na kupunguza kucha zake." Na katika tamko jingine: "...basi kamwe asichukue chochote katika nywele zake wala katika kucha zake mpaka atakapochinja dhabihu wa Idi."[2]

4- Takbira (kusema: Allaahu Akbaru), na tahlil (Laa ilaaha illa llaahu), na kumtaja Mwenyezi Mungu ndani

---

[1] Kaipokea Tirmidhi.
[2] Kaipokea Muslim.

ya siku hizi kumi na siku za Tashriiq (kubanika nyama); kwa hadithi ya Abdallah bin Omari, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao, kutoka kwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kwamba alisema: "Hakuna siku tukufu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu wala zinazopendeza zaidi kufanya matendo ndani yake, kuliko siku hizi kumi (za mwanzo za Dhul-Hija). Basi zidisheni sana ndani yake: Tahlili - yaani kusema: Laa ilaaha illa llaah (hakuna mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu), na Takbiri - yaani kusema: Allaahu Akbaru (Mwenyezi Mungu ni Mkubwa), na Tahmidi - yaani kusema: Alhamdulillaah (sifa njema ni za Mwenyezi Mungu)."[1]

Na takbira zina aina mbili, kama ifuatavyo:

Aina ya kwanza: Takbira za moja kwa moja. Nazo ni zile ambazo hazihusiani na baada ya swala; bali zinaruhusika nyakati zote.

Zinaanza takbira zisizo na mipaka katika Idil-Adhha kuanzia siku ya kwanza ya siku kumi (za mwanzo) za Dhul-Hija mpaka siku ya mwisho katika siku za Tashriiq (kubanika nyama), katika nyakati zote: usiku, mchana, barabarani, sokoni, msikitini, nyumbani na maeneo yote yanayofaa ndani yake kutajwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Aina ya pili: Takbira zenye mipaka: Nazo ni zile

---

[1] Kaipokea Ahmad.

zinazofungamanishwa na swala katika idil-Adhha hasa. Na wakati wake na namna yake ni kama ifuatavyo:

Kwanza: Zitaanza takbira zenye mipaka baada ya swala ya Alfajiri siku ya Arafa, na zitamalizika baada ya swala ya Laasiri siku ya tatu katika siku za Tashriiq (kubanika nyama). Hili ni kwa asiyekuwa hujaji. Na ama hujaji, yeye zitaanza takbira zenye mipaka kuanzia Adhuhuri ya siku ya kuchinja.

Pili: Namna ya kufanya takbira: Allaahu Akbaru, Allaahu Akbaru. Laa ilaaha illa llaahu, wallaahu Akbaru, Allaahu Akbaru walillaahil Hamd. Yaani: Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa. Hapana mungu apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mkubwa. Mwenyezi Mungu ni Mkubwa, na kila sifa njema ni zake Yeye Mwenyezi Mungu.[1]

5- Pupa ya kutekeleza swala ya Idi kwa asiyekuwa hujaji, kutoa takbira wakati wa kuiendea na kusikiliza hotuba. Kwani, hilo ni miongoni mwa alama kubwa za Uislamu. Na kwa sababu ya ukubwa wa jambo lake, wameamrishwa kuiendea wanawake mpaka mabikira na wenye hedhi. Imesimuliwa kutoka kwa Ummu Atwiya, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake,

[1] Tazama: Al-Mughni, cha bin Qudama 3/290, na Ashsharhul-Kabiir pamoja na Al-Muqni wal-Inswaaf 5/380.

kwamba alisema: "Tulikuwa tukiamrishwa kutoka siku ya Idi mpaka tukawa tunawatoa mabikira majumbani mwao wanamojihifadhi, vile vile mpaka tukawa tunawatoa wenye hedhi, nao wanakaa nyuma ya wanawake. Wakawa wanatoa takbira kwa takbira zao, na wanaomba kwa dua zao, na wanataraji baraka za siku hiyo na utakasifu wake." Na katika tamko jingine: "Na aliwaamrisha wenye hedhi wajitenge mbali na mahali wanaposwalia Waislamu."[1]

6- Kukithirisha matendo mema, miongoni mwa ibada za sunna: Kama vile swala, sadaka, kusoma Qur'ani Tukufu, kuamrisha mema na kukataza mabaya, kumtendea wema jirani, kuunga udugu na mengineyo miongoni mwa matendo mema, kwa ujumla wa kauli yake rehema na amani ziwe juu yake: "Hakuna siku ambazo kufanya matendo mema ndani yake hupendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko hizi siku kumi." Wakasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hata kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu?" Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani ziwe juu yake: "Hata kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa mtu aliyetoka kwa nafsi yake na mali yake, na akawa hakurudi na chochote katika hivyo."[2]

[1] Ameipokea Bukhari na Muslim.
[2] Kaipokea Bukhari na Tirmidhi, na tamko hili ni lake.

Na Mwenyezi Mungu pekee ndiye mwenye kuombwa atunufaishe kwa yale tuliyojifunza, na atufunze yale yenye kutunufaisha. Hakika Yeye ndiye Mpaji, Mkarimu. Na rehema na amani nyingi zimuendee Nabii wetu Muhammadi na watu wake.

❊❊❊

# Yaliyomo

FADHILA ZA SIKU KUMI (ZA MWANZO) ZA DHUL-HIJA..........2
Utangulizi..........2
Fadhila za siku kumi (za mwanzo) za Dhul-Hija: ..........3
Matendo bora zaidi katika siku kumi (za mwanzo) za Dhul-Hija: ..........4

❇❇❇

رئاسة الشؤون الدينية
بالمسجد الحرام والمسجد النبوي

رسالة الحرمين

# Ujumbe wa Haramain

Maudhui ya mwongozo kwa wanaokusudia Msikiti wa Haram na Msikiti wa Nabawi kwa lugha.

978-603-517-517-3